

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS –TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI IFAKARA



TAREHE: 20/05/2020

TANGAZO LA ZABUNI
NAMBA YA ZABUNI LGA/174/2020-2021/NC/01
ZABUNI YA UKUSANYAJI USHURU MBALIMBALI WA VYANZO VYA MAPATO
KWA MWAKA 2020/2021 KWA NJIA YA WAKALA

Halmashauri ya Mji Ifakara inakusudia kuweka wazabuni wa Utozaji Ushuru wa vyanzo mbalimbali vya mapato kwa mwaka 2020/2021.

Halmashauri ya Mji Ifakara inapenda kuwaalika watu Binafsi, Makampuni, Ushirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria, wenye nia na uwezo wa kufanya kazi hizo, watume maombi yao kwa zabuni zifuatazo:-

NA.	AINA YA ZABUNI	NAMBA YA ZABUNI	ENEO LA KUKUSANYA USHURU
1.	USHURU WA MAZAO YA CHAKULA NA NAFKA.	LGA/174/2019/2020/NC/01 LOT 01	ENEO LOTE LA TARAFI YA IFAKARA (KATA ZOTE TISA) HALMASHAURI YA MJI IFAKARA.
2.	USHURU WA MAZAO YA MISITU. (MBAO, MCAA, NGUZO, MIRUNDA, MAGOGO, KUNI NA MAZAO MENGINE YA MISITU.)	LGA/174/2019/2020/NC/01 LOT 02	ENEO LOTE LA HALMASHAURI YA MJI IFAKARA.
3.	USHURU WA STENDI YA MABASI (Stendi ya Kibaoni na Stendi ya kwa Makali)	LGA/174/2019/2020/NC/01 LOT 03	ENEO LA KATA YA KIBAONI NA KATA YA IFAKARA.
4.	USHURU WA VYOO. (Choo cha stendi ya mabasi kibaoni, kwa makali, soko kuu Ifakara na choo cha Viwanja	LGA/174/2019/2020/NC/01 LOT 04	ENEO LA (KATA YA IFAKARA (KATA YA KIBAONI NA KATA YA

	Sitini)		VIWANJA SITINI HALMASHAURI YA MJI IFAKARA.
5.	USHURU WA SAMAKI.	LGA/174/2019/2020/ NC/01 LOT 05	ENEO LOTE LA HALMASHAURI YA MJI IFAKARA ISIPOKUWA LESENI YA UVUVI/CHOMBO ITATOLEWA NA MAMLAKA HUSIKA.
6.	USHURU WA MADINI YA UJENZI (Mchanga ,Udongo,Mawe, Tofali na kokoto)	LGA/174/2019/2020/ NC/01 LOT 06	ENEO LOTE LA TARAFI YA IFAKARA (KATA ZOTE TISA) HALMASHAURI YA MJI IFAKARA.
7.	USHURU WA LESENI YA VYOMBO VYA USAFIRI NA MIZIGO (STIKER)	LGA/174/2019/2020/ NC/01 LOT 07	ENEO LOTE LA HALMASHAURI YA MJI IFAKARA.

MASHARTI YA MAOMBI YA ZABUNI


Maombi yote ya zabuni yazingatie masharti yafuatayo:-

1. Nyaraka za zabuni zitapatikana baada ya kulipa ada ya kila zabuni husika. Ada hiyo haitarejeshwa (Non refundable). Mwombaji atalipa ada ya maombi ya Tshs. **100, 000/=** Kwa kila zabuni, fedha zilipwe baada ya kupata kifungu cha kulipia (Control number) kutoka Ofisi ya Mweka Hazina wa Halmashauri ya Mji Ifakara.
2. Ombi la zabuni liwe na jina la zabuni anayoomba, aidha aonyeshe mahali ofisi yake ilipo.
3. Mwombaji atatakiwa kuambatanisha kivuli cha leseni ya biashara iliyo hai, kivuli cha usajili wa kampuni, usajili wa VAT/TIN na uwakilishi kisheria "Power of Attorney" pamoja na miamala ya benki (bank statement) ya miezi mitatu kabla ya tarehe ya tangazo hili, pia aambatanishe na wasifu wa kampuni "Company Profile" ya kampuni hiyo.
4. Mwombaji atatakiwa kutoza viwango halali vilivyoidhinishwa na Sheria mama na Sheria Ndogo za Halmashauri ya Mji Ifakara.
5. Mwombaji aoneshe kiwango cha fedha atakacholipa kwa Halmashauri kwa kila Zabuni,

6. Iwapo mzabuni atachaguliwa, atatakiwa kuwasilisha dhamana utendaji "Performance guarantee" ya malipo ya miezi miwili (2) na wadhamini wawili wenye mali zisizohamishika na wanaotambulika, kabla ya kusaini mkataba.
7. Mwombaji aorodheshe vifaa alivyonavyo, idadi ya wafanyakazi na uzoefu wao. Pia mwombaji aoneshe uzoefu alionao katika zabuni hiyo.
8. Mwombaji aandike juu ya bahasha na kwenye barua ya maombi, aina na namba ya zabuni anayoomba. Atatakiwa kutuma kabrasha halisi (original) na nakala (copy) mbili (2) na yawekwe kwenye bahasha moja. Juu ya bahasha kusiandikwe wala kuwekwa alama yoyote zaidi ya jina la zabuni, namba ya zabuni na anuani ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Ifakara.
9. Mwombaji atoe tamko la kutojihusisha na vitendo vya rushwa.
10. Halmashauri haitalazimika kukubali zabuni ya bei ya chini isipokuwa kwa vigezo muhimu vilivyopo katika tangazo hili na kabrasha la zabuni.
11. Maombi yafungwe kwenye bahasha ya khaki kwa lakiri na kutumwa kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni kwa anuani ifutavyo:-

**Katibu wa Bodi ya Zabuni,
Halmashauri ya Mji Ifakara,
S.L.P 433, IFAKARA.**

12. Kabrasha la zabuni linapatikana katika ofisi za Halmashauri ya Mji Ifakara
13. Mwisho wa kupokea maombi hayo ni **tarehe 02/06/2020 saa sita (6) mchana**. Waombaji au wawakilishi wao, wanaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni hizo utakaofanyika katika ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Mji Ifakara. Aidha, unashauriwa kutembelea eneo la kazi ndani ya Halmashauri ya Mji Ifakara kabla ya kuleta maombi.
14. Mzabuni hatahusika na utoaji wa vibali, lesseni mbalimbali, zitatolewa na mamlaka husika.
15. Mzabuni atatumia mashine za kukusanyia mapoto (POS)


Francis K. Ndulane
**MKURUGENZI WA MJI
IFAKARA**

